JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA UNUNUZI WA UMMA**

PPRA
Public Procurement Regulatory Authority

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. No. FB.192/247/01/B/27** **9 Julai, 2025**

**Kwa Taasisi Nunuzi zote; na**
**Wadau wa Ununuzi wa Umma.**

Yah: **KALENDA YA MAFUNZO YA MATUMIZI YA SHERIA YA UNUNUZI WA UMMA YA MWAKA 2023 NA KANUNI ZAKE ZA MWAKA 2024 NA MFUMO WA KIELEKTRONIKI WA UNUNUZI WA UMMA (NeST)**

Tafadhali rejea kichwa cha habari hapo juu.

2. Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma inalo jukumu la kuamua, kuendeleza, kuanzisha, kutunza na kuhuisha mfumo husika wa kuwezesha ununuzi wa umma kwa njia ya teknolojia za habari na mawasiliano, ikijumuisha matumizi ya mfumo wa kielektroniki katika usimamizi wa ununuzi na ugavi. Aidha, Mamlaka inalojukumu pia la kuwajengea uwezo wadau wanaoshiriki katika masuala ya ununuzi na ugavi wa umma.

3. Hivyo, kufuatia maboresho makubwa katika Sheria ya Ununuzi wa umma ya mwaka 2023 pamoja na kutengenezwa kwa moduli mbalimbali za Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST), Mamlaka imeandaa Kalenda ya Mafunzo ya mwaka 2025/2026 ambayo yataanza kutolewa Mwezi Agosti, 2025. Kwa barua hii Mamlaka inatangaza ratiba ya Mafunzo kutokana na mahitaji ya watumiaji kama inavyoonekana kwenye ratiba iliyoambatanishwa.

4. Mafunzo ya pamoja ya kutumia mfumo yatatolewa kwa muda wa siku tano (5) kwa Taasisi Nunuzi na Siku moja (1) kwa Wazabuni; na mafunzo ya matumizi ya Sheria, Kanuni pamoja na Uandaaji wa Nyaraka za Zabuni ndani ya mfumo yatatolewa kwa muda wa siku nne (4). Ada kwa kila mshiriki kutoka Taasisi Nunuzi ni **TZS 600,000.00**; na **TZS 100,000.00** kwa kila mshiriki kutoka kwa Wazabuni.

5. Maafisa Masuuli wanahimizwa kushiriki mafunzo haya na kuwaruhusu watumishi wao kuhudhuria mafunzo watakayochagua kushiriki kwa mujibu wa Kalenda ya Mafunzo

3 Barabara ya Ununuzi , S.L.P 2865, 41104 TAMBUKARELI Dodoma, TANZANIA
Simu: +255 26 2963854, Barua pepe: dg@ppra.go.tz, Tovuti: www.ppra.go.tz

Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma

iliyoambatanishwa pamoja na mwaliko huu, ambayo pia inapatikana katika tovuti ya PPRA kupitia www.ppra.go.tz na mfumo wa mafunzo unaopatikana kupitia https://tsms.ppra.go.tz.

6. Ili kushiriki mafunzo, kila mshiriki anapaswa kujisajili katika mfumo wa mafunzo (https://tsms.ppra.go.tz), kwa kuchagua mafunzo anayotaka kushiriki na kuthibitisha ushiriki kwa kulipia ada ya mafunzo kupitia Namba ya Malipo (Control Number) inayotolewa na mfumo wa mafunzo (tsms) kulingana na aina ya mafunzo husika. Iwapo taasisi itahitaji Namba ya malipo ya pamoja kwa washiriki zaidi ya mmoja, huduma hii inapatikana katika mfumo wa mafunzo wa (TSMS) eneo la "*Group Bill*"

7. Tunashukuru kwa ushirikiano wenu.

Dennis K. Simba
**MKURUGENZI MKUU**

Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma